**SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI ZANZIBAR NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**UANZISHWAJI WA TAASISI**

3. Uanzishwaji wa Taasisi.
4. Muhuri na Nembo ya Taasisi.
5. Kazi za Taasisi.
6. Uwezo wa Taasisi.

**SEHEMU YA TATU**
**USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA TAASISI**

7. Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.
8. Sifa za Mwenyekiti.
9. Katibu wa Bodi.
10. Kazi za Bodi.
11. Uwezo wa Bodi.
12. Mwenendo wa Bodi.
13. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.
14. Sifa za Mkurugenzi Mkuu.

15. Idara, divisheni na vitengo.

16. Wafanyakazi wa Taasisi.

**SEHEMU YA NNE**
**UENDESHAJI WA TAASISI**

17. Uanzishwaji wa maabara.

18. Maeneo ya utafiti wa uvuvi na maliasili za baharini.

19. Masharti ya kufanya utafiti.

20 Mashirikiano.

21. Uvumbuzi na ubunifu.

22. Umiliki wa uvumbuzi na ubunifu.

23. Zawadi za uvumbuzi na ubunifu.

24. Taarifa kuwasilishwa kwa Taasisi.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI YA FEDHA**

25. Fedha na rasilimali za Taasisi.

26. Bajeti ya Taasisi.

27. Hesabu na Ukaguzi.

**EHEMU YA SITA**
**MAKOSA NA ADHABU**

28. Makosa na adhabu.

29. Adhabu ya ujumla.

30. Kumaliza kosa.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI MENGINEYO

31. Kanuni za Maadili.

32. Mipaka ya haki ya kutoa taarifa.

33. Marekebisho ya majaduweli.

34. Kanuni.

## JADWELI

**SHERIA NAM. 11 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

1 Februari, 2024

# SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI ZANZIBAR NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar ya 2023 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitajika vyenginevyo:

"bidhaa za maji ya baharini na maji baridi" maana yake ni ya bidhaa yoyote ya chakula au nyuzi zinazopatikana kutokana na uvuvi au ukuzaji wa viumbe maji;

"bidhaa za samaki" maana yake ni kitu chochote kilichotengenezwa, kilichokusanya au kupatikana kutokana na samaki ikiwemo samaki, samaki wakavu, mbolea ya samaki na mapambo, samaki wabichi, mbolea itokanayo na samaki, matumbo ya samaki, majimaji yatokanayo na samaki, mafuta

ya samaki, lulu, sehemu ya ndani ya ngamba la chaza, magamba ya samaki au chaza, chakula kitokanacho na jongoo bahari, girisi au nta itokanayo na samaki, viluivuli vya samaki na sposhi la baharini;

"bidhaa za uvuvi" maana yake ni kitu chochote kilichotengenezwa, kilichotolewa au kupatikana kutoka kwa samaki na viumbe wengine wanaoishi baharini au maji baridi;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7(1) cha Sheria hii;

"Kituo cha Utafiti" maana yake ni kituo kilichoanzishwa kwa lengo la kutoa uzoefu, utafiti, ubunifu, msaada na mafunzo juu ya fani makhsus;

"kuvua" maana yake ni kitendo cha kukusanya, kukamata, kuvuna, kuua au kutega samaki, bidhaa za samaki au wanyama na mimea ya baharini na maji baridi;

"Maji ya kitaifa" maana yake ni maji ya ndani ya eneo linaloongezeka baharini katika masafa ya meli kumi na mbili kutoka katika mstari wa asili wa mwambao wa kina kidogo.

"Maji ya ndani" maana yake ni eneo lolote la baharini ambalo lipo upande wa ardhini kutoka katika mstari wa asili unaoyagawa maji ya baharini ya kitaifa;

"maliasili za baharini" maana yake ni maliasili zote ambazo kwa asili zinapatikana katika mazingira ya baharini zenye thamani ya kimaumbile au kifedha;

"mimea ya maji ya baharini na maji baridi" maana yake ni mimea yote inayostawi na kukua katika mazingira ya maji ya baharini na maji baridi;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 13(1) cha Sheria hii;

"Mtafiti wa kigeni" maana yake ni mtafiti ambaye sio raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"samaki" maana yake ni aina zote za wanyama wa maji ya baharini au maji baridi ikijumuisha samaki wenye mapezi, samaki wasio na mapezi, samaki jamii ya chaza, nguva, kasa, pomboo na nyangumi pamoja na mayai, vifaranga na watoto wao;

"sayansi za baharini" maana yake ni elimu ya bahari, maarifa na ujuzi kuhusu baharini, viumbe vya baharini na maisha yao na tabia zao, kemia ya baharini, mienendo na mifumo ya baharini, miamba na sakafu ya baharini na maumbile yake;

"Taasisi" maana yake ni Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar kama iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria hii;

"ukuzaji wa viumbe maji" maana yake ni ukulima au juhudi za kuzalisha, kukuza na kuvuna wanyama na mimea katika mazingira ya maji ya baharini au maji baridi;

"uvuvi" maana yake ni sehemu inayohusiana na shughuli zilizomo katika tasnia ya uvuvi ikijumuisha, vifaa vya utaalamu kisayansi, matendo, usarifu au mifumo kuhusiana na:

(a) biashara ya uvuvi;

(b) ujenzi au utengenezaji wa mabwawa ya uzalishaji samaki au mashamba ya samaki kwa lengo la kuvuna au kuwezesha upatikanaji wa samaki,

(c) utengenezaji wa vitu vinavyotumika katika uvuvi au kwa madhumuni ya tasnia ya uvuvi;

(d) udhibiti wa uvuvi;

(e) ubunifu, utoaji na uwekaji wa haki za kuvua;

(f) uzalishaji au uongezaji wa idadi ya samaki;

(g) utayarishaji wa vyakula vya samaki, utengenezaji au uumiaji wa bidhaa za samaki; na

(h) uchunguzi, ukingaji au udhibiti wa mripuko wa maradhi ya samaki;

"wanyama wa maji ya baharini na maji baridi" maana yake ni wanyama wote wanaoishi na kustawi katika mazingira ya maji ya baharini na maji baridi;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na uvuvi;

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI WA TAASISI

Uanzishwaji wa Taasisi.

3.-(1) Kunaanzishwa Taasisi itakayojulikana kama Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na ufupisho wake itakuwa "ZAFIRI".

(2) Taasisi itakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye urithi wa kuendelea, chenye muhuri na kwa jina lake kwa mujibu wa sheria zinazotumika zitakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa

(b) kupata, kumiliki, kununua au kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba au muamala wowote;

(d) kukopa, kukopesha au kupokea msaada wa kiwango chochote cha fedha kutoka katika taasisi yoyote ya kifedha; na

(e) kutekeleza au kutenda jambo lolote ambalo Taasisi kwa asili yake inaweza kufanya kisheria.

Muhuri na Nembo ya Taasisi.

4.-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Taasisi katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Taasisi katika nyaraka yoyote itathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mkuu au afisa mwengine yeyote wa Taasisi aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Taasisi utawekwa muhuri wa Taasisi na utathibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Taasisi.

5.-(1) Taasisi itakuwa na jukumu la kufanya utafiti na ubunifu wa uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na maliasili za baharini ndani ya Zanzibar na eneo jengine lolote ambalo litakuwa na faida kwa Zanzibar.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Taasisi:

(a) itafanya utafiti katika uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na maliasili za baharini,

(b) itawezesha uratibu wa utafiti, uvumbuzi na ubunifu katika uvuvi na maliasili za baharini kwa kushauriana na taasisi husika;

(c) itaendeleza na kukuza utafiti, teknolojia na ubunifu kwa ajili ya kuvua, ukuzaji wa viumbe maji, kusarifu samaki na mazao yatokanayo na viumbe maji, na usimamizi na uhifadhi wa maliasili za baharini na ekelojia ya baharini;

(d) itawasilisha na kusambaza ujuzi na matokeo ya utafiti yanayohusiana na uvuvi na maliasili za baharini;

(e) itahamasisha na kuwezesha matumizi ya matokeo ya utafiti;

(f) itaunganisha kazi za utafiti wa uvuvi, maliasili za baharini, ekolojia ya baharini na sayansi ya baharini kwa matumizi ya umma;

(g) itapata, itahifadhi na kusambaza taarifa za kisayansi na teknolojia kuhusiana na usimamizi wa uvuvi, uhifadhi wa maliasili za baharini, ekolojia na sayansi za baharini;

(h) itashirikiana na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa katika kufanya utafiti wa uvuvi, rasilimiali za baharini, ekolojia ya baharini na sayansi za baharini;

(i) itatoa huduma za kimaabara ili kuthaminisha ubora wa samaki, bidhaa za samaki na bidhaa nyengine za baharini na maji baridi;

(j) itakuza ubora wa bidhaa za baharini, utunzaji kabla na baada ya kuvuna, teknolojia na ubunifu wa kuongeza thamani;

(k) itashauri na kutoa mapendekezo kwa Waziri katika mambo yanayohusiana na kazi za Taasisi;

(l) itatoa huduma za ushauri elekezi zinazohusiana na maendeleo na usimamizi wa uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji;

(m) itaainisha maeneo ya utafiti ya uvuvi, maliasili za baharini na maeneo mengine ya sayansi za baharini kwa kushauriana na taasisi husika;

(n) italea na kukuza watafiti wapya katika uvuvi, maliasili za baharini na sayansi nyengine za baharini; na

(o) itatekeleza kazi nyengine yoyote ambayo inayohusiana na kazi za Taasisi kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

Uwezo wa Taasisi.

6. Taasisi itakuwa na uwezo wa:

(a) kutoa miongozo kwa ajili ya kufanya shughuli za utafiti katika uvuvi, maliasili za baharini na sayansi za baharini itakayotumika na taasisi inayohusika na utoaji wa kibali cha utafiti;

(b) kutoa Cheti cha Maadili na Miiko ya Utafiti kilichoidhinishwa kwa ajili ya utafiti wa uvuvi na maliasili na baharini;

(c) kuanzisha vituo ndani ya Taasisi kwa ajili ya kukuza utafiti na ubunifu; na

(d) kuingia katika mashirikiano ya maendeleo ya utafiti unaohusiana na baharini.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA TAASISI

Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.

7.-(1) Kunaanzishwa Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi.

(2) Bodi itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Mkurugenzi anayehusika na Uvuvi;

(d) Mkurugenzi anayehusika na Uhifadhi wa Baharini;

(e) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

(f) mjumbe mmoja kutoka taasisi ya elimu ya juu ambaye ni mtaalamu katika uvuvi au maliasili za baharini; na

(g) mjumbe mmoja kutoka sekta binafsi anayehusika na uvuvi au maliasili za baharini.

(3) Wajumbe chini ya aya ya (e), (f) na (g) watateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia taaluma, jinsia na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika fani husika.

Sifa za Mwenyekiti.

**8.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza au inayolingana katika fani yoyote kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika fani hiyo; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Katibu wa Bodi.

**9.**-(1) Bodi itamteua mfanyakazi wa Taasisi kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria au mwenye sifa ya kuwa katibu wa shirika kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali; na

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na:

(a) ataandaa ajenda za vikao kwa kushauriana na Mwenyekiti;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza taarifa sahihi na zinazojitosheleza za vikao ya Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi ya vikao vya Bodi kwa wajumbe; na

(e) atafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi kwa mujibu wa Sheria hii.

Kazi za Bodi.

**10.** Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia, kuelekeza na kutoa miongozo juu ya masuala ya Taasisi;

(b) kutoa miongozo juu ya utayarishaji na utekelezaji wa sera ya utafiti wa uvuvi na maliasili za baharini;

(c) kusimamia mali, biashara, fedha na masuala mengine ya Taasisi;

(d) kumshauri Waziri juu ya masuala yanayohusiana na utafiti wa uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji, maliasili za baharini na sayansi za baharini; na

(e) kufanya kazi nyengine yoyote itakayoonekana ni muhimu kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Sheria hii.

Uwezo wa Bodi.

**11**.-(1) Bodi itakuwa na uwezo wa jumla katika kusimamia utekelezaji wa kazi za Taasisi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi itakuwa na uwezo wa:

(a) kuajiri wafanyakazi wa Taasisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(b) kupendekeza muundo wa utumishi wa Taasisi kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(c) kuidhinisha ada na tozo nyengine za huduma zinazotolewa na Taasisi;

(d) kutoa muongozo na kuidhinisha ajenda za utafiti wa Taasisi;

(e) kuidhinisha bajeti ya Taasisi;

(f) kuidhinisha mpango mkakati, mipango ya mwaka na miongozo mengine ya Taasisi;

(g) kuandaa Kanuni za Maadili ya Utafiti wa Uvuvi na Sayansi za Baharini;

(h) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mfanyakazi yeyote wa Taasisi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

Mwenendo wa Bodi.

**12**. Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

**13.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mkurugenzi Mkuu atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi na atakuwa na wajibu wa usimamizi wa kazi za kila siku za Taasisi.

Sifa za Mkurugenzi Mkuu.

**14.**Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sayansi ya baharini, uvuvi au fani nyengine yoyote inayolingana na hizo kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika fani hiyo; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Idara, divisheni na vitengo.

**15.**-(1) Taasisi inaweza, kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake chini ya Sheria hii, kuanzisha idara, divisheni na vitengo kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Wakuu wa idara watateuliwa na Bodi kulingana na sifa na uzoefu wao.

(3) Wakuu wa divisheni na vitengo watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kulingana na sifa na uzoefu wao.

(4) Wakuu wa idara, divisheni na vitengo watawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu.

Wafanyakazi wa Taasisi.

**16.** Kutakuwa na wafanyakazi wa Taasisi ambao wataajiriwa chini ya vigezo na masharti kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

## SEHEMU YA NNE
## UENDESHAJI WA TAASISI

Uanzishwaji wa maabara.

**17.** Bila ya kuathiri masharti ya sheria nyengine yoyote inayotumika, Taasisi itaanzisha maabara kwa ajili ya kudhibiti ubora wa samaki na bidhaa za uvuvi ili kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii.

Maeneo ya utafiti wa uvuvi na maliasili za baharini.

**18.**-(1) Utafiti wa uvuvi na maliasili za baharini utakaofanywa na Taasisi utalenga katika maeneo mbali mbali kama zilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii.

(2) Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Bodi na kwa tangazo litakalochapishwa katika Gazeti, kutangaza maeneo mapya ya utafiti.

Masharti ya kufanya utafiti.

**19.**-(1) Mtafiti ambaye anakusudia kufanya utafiti chini ya Sheria hii, baada ya kufanya maombi kwa Taasisi, atapewa Cheti cha Maadili na Miiko ya Utafiti.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, vigezo na masharti ya kupata Cheti cha Maadili na Miiko ya Utafiti yataelezwa katika kanuni.

Mashirikiano.

**20.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Taasisi itashirikiana na taasisi nyengine katika hatua za utoaji wa vibali vya utafiti wa uvuvi na utafiti wa maliasili za baharini.

(2) Taasisi itawezesha utafiti wa uvuvi na maliasili za baharini kwa kushirikiana na taasisi nyengine za umma na binafsi.

Uvumbuzi na ubunifu.

**21.**-(1) Taasisi inaweza, kwa madhumuni ya kuingia katika biashara ya uvumbuzi na ubunifu wowote ambao Taasisi itaona ni muhimu katika kuimarisha uvuvi na usimamizi wa maliasili za baharini, kukubaliana na mmiliki wa uvumbuzi huo kununua au kuuza uvumbuzi wowote unaohusiana na uvuvi au maliasili za baharini kwa kuzingatia vigezo na masharti kama itakavyoweza kuamuliwa na Taasisi.

(2) Kila uvumbuzi na ubunifu uliofanyika kutokana na uvuvi na sayansi za baharini au utafiti mwengine wa kisayansi uliyofanywa chini ya Sheria hii utasajiliwa na Taasisi katika namna na masharti kama itakavyoainishwa katika kanuni.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, taasisi itatoa miongozo ya uvumbuzi na ubunifu wa uvuvi, maliasili za baharini na sayansi za baharini.

Umiliki wa uvumbuzi na ubunifu.

**22.**-(1) Uvuvi na maliasili zote za baharini zinazohusiana na uvumbuzi na ubunifu uliyofanywa na Taasisi wakati wa utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii, utakuwa ni miliki ya Taasisi na Taasisi inaweza kuuweka wazi uvumbuzi na ubunifu huo kwa umma.

(2) Taasisi inaweza, kwa idhini ya Bodi:

(a) kutoa tunzo au mirabaha kama itakavyoona inafaa, kwa mtu yeyote ambaye amefanya uvumbuzi au ubunifu kutokana na utafiti wowote uliofanywa, au ulioelekezwa kufanywa na Taasisi, ikiwa mtu huyo ni mwajiriwa wa Taasisi au vyenginevyo; na

(b) kumsamehe mtu yeyote kutolipa ada endapo uvumbuzi au ubunifu umewekwa wazi kwa umma kwa malipo ya ada au mrabaha.

Zawadi za uvumbuzi na ubunifu

23. Taasisi itampa zawadi mtu yeyote ambaye atapeleka uvumbuzi au ubunifu **wowote** utakaopelekea maendeleo ya sekta ya uvuvi na usimamizi wa maliasili za baharini.

Taarifa kuwasi-lishwa kwa Taasisi.

24. Mtafiti, ndani ya muda utakaoamuliwa na Taasisi, kwa gharama zake, atawasilisha taarifa zote muhimu kwa Taasisi zinazohusiana na utafiti huo na kuweka wazi kwa Taasisi data, kumbukumbu, matokeo au ripoti husika ya utafiti.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali za Taasisi.

25.-(1) Fedha na rasilimali za Taasisi zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha zozote halali zilizopokelewa na Taasisi kutokana na huduma zinazotolewa na Taasisi;

(c) misaada halali, zawadi, michango, mikopo, urithi au uwekezaji kama Taasisi itakavyopokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote; na

(d) fedha nyengine zozote ambazo zinaweza kupewa au kupatikana kihalali na Taasisi wakati wa utekelezaji wake au vyenginevyo.

(2) Taasisi itatekeleza kazi zake kwa mujibu wa msingi ya kifedha iliyopo na itahakikisha kwamba mapato yake yanajitosheleza kufikia matumizi yake ipasavyo.

(3) Taasisi inaweza kubakiza asilimia fulani ya fedha zilizokusanywa kama itakavyoamuliwa na Waziri anayehusika na Fedha.

(4) Miamala yote ya fedha ya Taasisi itafanywa na itasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

Bajeti ya Taasisi.

26.-(1) Mkurugenzi Mkuu, katika kila mwaka wa fedha, ataanda na kuwasilisha kwa Bodi kwa ajili ya majadiliano na mapendekezo ya makadirio ya kina ya mapato na matumizi ya Taasisi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Baada ya majadiliano na mapendekezo ya Bodi, bajeti ya Taasisi itachukuliwa kuwa ni sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Makadirio ya mapato na matumizi ya Taasisi yataandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016 na miongozo mingine yoyote takayotolewa na Serikali kila baada ya muda.

(4) Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba malipo yote yanayofanywa kwa fedha za Taasisi ni sahihi na yanaidhinishwa ipasavyo, na udhibiti wa kutosha utadumishwa juu ya mali na madeni ya Taasisi.

Hesabu na Ukaguzi.

27.-(1) Taasisi itaweka na kutunza kwa usahihi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.

(2) Hesabu zote za Taasisi zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 na sheria nyengine zozote za fedha zinazohusika.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu.

28. Mtu yeyote ambaye:

(a) ametoa taarifa za uongo au zisizo sahihi ambazo zitakwaza utekelezaji wa kazi za utafiti wa uvuvi na maliasili za baharini;

(b) ameingilia utekelezaji wa utafiti wa uvuvi unaofanywa chini ya Sheria hii;

(c) amemzuia au amemkwaza afisa wa utafiti wa uvuvi na maliasili za baharini katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii;

(d) amehamisha matokeo ya utafiti ya Taasisi bila ya ruhusa ya Taasisi;

(e) ameathiri auameharibu mali au shughuli yoyote inayohusiana na utafiti wa uvuvi na maliasili za baharini chini ya Sheria hii;

(f) amefanya utafiti bila ya Cheti cha Maadili ya Miiko ya Utafiti kilichotolewa na Taasisi; na

(g) ameshidwa kufuata masharti yoyote ya Sheria hii,

ametenda kosa, na akitiwa hatiani:

(a) ikiwa ni mtafiti binafsi, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania; au

(b) ikiwa ni taasisi, italipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Ishirini za Kitanzania.

Adhabu ya ujumla.

**29**. Mtu yeyote ambaye atakwenda kinyume na masharti yoyote ya Sheria hii, ambapo hakuna adhabu maalum iliyowekwa kwa kosa hilo ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania.

Kumaliza kosa.

**30**.-(1) Mkurugenzi Mkuu anaweza kumaliza kosa lililofanywa na mtu chini ya Sheria hii au kanuni zake kwa kumtaka kulipa faini isiyopungua nusu ya faini iliyoainishwa kwa kosa hilo, iwapo mtu huyo:

(a) amekubali kwamba ametenda kosa na atachukua tahadhari kwa kutorudia tena kosa; na

(b) atalipa malipo yote ambayo hayajalipwa chini ya Sheria hii.

(2) Taratibu zinazohusiana na kumaliza kosa zitaainishwa katika kanuni.

(3) Kumaliza kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hautochukuliwa kama ni hatia kwa kosa linaloshukiwa kufanywa na isipokuwa kwamba malipo ya faini ya msingi yamelipwa yote, hakutokuwa na mashtaka kwa kosa ambalo litafunguliwa au kuendelezwa.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI MENGINEYO

Kanuni za Maadili.

**31**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Taasisi itaandaa Kanuni za Maadili za Utafiti wa Uvuvi na Sayansi za Baharini.

(2) Taasisi itahakikisha kwamba utafiti unafanywa kwa mujibu wa maadili na viwango kama itakavyoainishwa katika miongozo

Mipaka ya haki ya kutoa taarifa.

**32**. Taasisi, isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo na sheria, haitowajibika kutoa taarifa zozote ambazo kwa maoni ya Taasisi, zitaathiri uadilifu katika kufanya kazi zake.

Marekebisho ya Majadweli.

**33**. Waziri anaweza, kwa amri iliyochapishwa katika Gazeti, kurekebisha Jadweli lolote chini ya Sheria hii.

Kanuni.

**34**.-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti chini ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga kanuni katika mambo yafuatayo:

(a) usimamizi na udhibiti wa data, taarifa, matokeo ya utafiti, uvumbuzi na ubunifu;

(b) kuweka ada na tozo kwa ajili ya huduma zinazotolewa na Taasisi; na

(c) taratibu za kutoa Cheti cha Miiko na Maadili ya Utafiti.

Kufuta na kubakiza.

**35**.-(1) Tangazo la Kisheria Nambari 32 la mwaka 2019 linafutwa.

(2) Jambo lolote halali lililofanywa au limedaiwa kufanyika chini ya Tangazo Nambari 32 la mwaka 2019 kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, litachukuliwa kuwa limefanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

---

## MWENENDO WA BODI
**[Chini ya kifungu cha 12]**

---

Makamu Mwenye-kiti.

1. Wajumbe wa Bodi watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Muda wa wajumbe.

2. Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

3.-(1) Bodi itakutana kikawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana kwa ajili ya kikao cha dharura muda wowote kila itakapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

(2) Mwenyekiti ataendesha vikao vyote vya Bodi, na ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha vikao vya Bodi na ikiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliohudhuria watachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

4. Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wa Bodi wataunda akidi katika kikao cha Bodi.

Maamuzi ya Bodi.

5. Uamuzi wa Bodi utafanywa kwa maafikiano, na endapo hakuna maafikiano, uamuzi utafanywa kwa kura, na endapo ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Taratibu za vikao.

6. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake.

Mjumbe mualikwa.

7. Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya vikao vya Bodi kama mtaalamu, lakini mjumbe mualikwa huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kamati za Bodi

8. Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati pale inapoona inafaa.

Kukasimu kazi za Bodi.

9.-(1) Bodi inaweza, itakapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa kamati za Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa maelekezo kwa maandishi kama itakavyoona muhimu kuhakikisha utekelezaji bora wa kazi zake.

Posho la Wajumbe.

10. Wajumbe wa Bodi watastahili kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

Kubainisha maslahi.

11.-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi binafsi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo ambalo linalohusika au linalotakiwa kujadiliwa na Bodi, haraka iwezekanavyo, baada ya kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha maslahi hayo:

(a) hatohudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya maamuzi; au

(b) hatomshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya maamuzi.

Kusita kuwa mjumbe.

12. Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatohudhuria vikao vitatu mfuiulizo vya Bodi bila ya sababu ya msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili;

(d) akisita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza mjumbe huyo;

(e) ikiwa atasitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Taasisi; au

(f) kifo.

## JADWELI LA PILI

## MAENEO YA UTAFITI
**[Chini ya kifungu cha 18(1)]**

1. Shughuli za kibinaadamu;
2. Uchumi wa ukuzaji wa viumbe maji;
3. Ramani ya maeneo sahihi ya shughuli za ukuzaji wa viumbe maji;
4. kolojia ya mazingira ya baharini na maji baridi na taarifa za baianuai;
5. Viumbe maji visivyo vya asili na vilivyohatarini kutoweka;
6. Uzalishaji wa viumbe maji na faida zao;
7. Baiinfomatiki;
8. Mahusiano baina ya samaki wasiokusudiwa kuvunwa na bioanuai;
9. Mabadiliko ya tabianchi;
10. Fedha za kusaidia mabadiliko ya tabianchi;
11. Athari katika matumbawe na maradhi katika kilimo cha mazao ya baharini;
12. Utalii wa kimaumbile;
13. Chakula na lishe;
14. Matumbawe bandia;
15. Uvuvi na kiwango cha samaki;
16. Maradhi ya samaki;
17. Teknololojia katika ufugaji wa samaki na usarifu;
18. Uvuvi wa samaki, usafirishaji, uhifadhi, masoko na ugavi;
19. Vitalu vya samaki, jinsia, usalama, teknolojia na vinasaba;
20. Mfumo wa usimamizi mazao ya baharini;
21. Uhamiaji wa wavuvi;
22. Zana na vifaa vya uvuvi;
23. Masuala ya jinsia katika uvuvi;
24. Hewa ukaa;
25. Teknolojia ya kuzalisha samaki;
26. Makosa haramu, yasiyoripotiwa, yasiyo ya kisheria;
27. Mazingira hatarishi;
28. Sayansi ya baharini;

29. Usimamizi na uhifadhi wa maliasili za mwambao na baharini;
30. Baiolojia na ikolojia ya baharini;
31. Usimamizi na kukabiliana na majanga ya baharini;
32. Ramani na mipango ya baharini;
33. Tindikali baharini;
34. Fisikia baharini;
35. Mapambo, vito na makumbusho baharini;
36. Sera, ushawishi na utawala katika uvuvi na mazao ya baharini;
37. Viashiria vya uchafuzi wa mazingira;
38. Idadi ya watu, afya na mazingira;
39. Kabila muhimu za samaki;
40. Umasikini na utumikishaji wa watoto katika jamii za uvuvi;
41. Kuchora ramani kwa kutumia satalaiti;
42. Utafiti na elimu ugani;
43. Uhimilivu kwa viumbe vya baharini;
44. Mizozo ya kijamii na kisekta;
45. Hali halisi ya maliasili za mwambao na baharini;
46. Uendelevu kwa maliasili za baharini;
47. Maendeleo ya teknolojia katika uvuvi na mazao ya baharini;
48. Kuongeza thamani na ubora wa bidhaa;
49. Uchambuzi katika mnyororo wa thamani;
50. Ubora wa maji, kiwango, upatikanaji na uchafuzi wa mazingira; na
51. Eneo jengine la utafiti ambalo Taasisi itaona ni muhimu.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 5 Disemba, 2023.

..........................................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
*Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.*